DSM GREEN ACRES SCHOOLS

O-Level and A-Level Secondary Schools
Located at Salasala - Mbezi Beach off Bagamoyo Road
Email: info@greenacres.ac.tz | **Website:**www.greenacres.ac.tz
P.O. BOX 105177, DAR ES SALAAM
Phone: +255 754 306 598 | +255 739 999 926 | +255 782 128 633 | +255 765 172 199

KUHUSU SHULE YETU

DSM Green Acres Schools ni shule za kutwa na bweni zilizopo Salasala, takribani kilomita 20 kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam. Tunatoa elimu bora katika mazingira tulivu, salama na rafiki kwa ujifunzaji, tukizingatia taaluma, nidhamu, maadili na ukuzaji wa vipaji vya kila mwanafunzi.

MAONO NA DHAMIRA YETU

Maono: Kuwa taasisi kinara katika kutoa elimu na malezi bora, inayowaandaa wanafunzi kuwa wenye maarifa, maadili mema, uzalendo na uwezo wa kushindana kimataifa.

Dhamira: Kutoa elimu bora inayokuza ufaulu wa kitaaluma, ubunifu, fikra tunduizi na uadilifu, ili kuwaandaa wanafunzi kukabiliana na changamoto za maisha.

MTAALA NA TAALUMA

Tunafuata Mtaala wa Taifa wa Tanzania kuanzia Elimu ya Awali, Msingi hadi Sekondari, huku Kiingereza kikiwa lugha kuu ya kufundishia. Tunasisitiza ufaulu bora, ujifunzaji kwa vitendo, matumizi ya teknolojia na uwezo wa mwanafunzi kufikiri, kubuni na kutatua changamoto.

MAZINGIRA NA MIUNDOMBINU

Shule zetu zina madarasa ya kisasa, maabara za sayansi na kompyuta, maktaba, viwanja vya michezo na mabweni salama yenye usimamizi wa karibu. Tunazingatia idadi ya wanafunzi isiyozidi 25 kwa darasa ili kuwezesha ufundishaji na ufuatiliaji wa kila mwanafunzi.

MICHEZO NA UKUZAJI WA VIPAJI

Tunatoa fursa mbalimbali za michezo, muziki, sanaa, maigizo, klabu za wanafunzi na ziara za kielimu. Shughuli hizi hujenga kujiamini, ubunifu, uongozi, ushirikiano na stadi muhimu za maisha.

AFYA, LISHE NA USALAMA

Afya na ustawi wa wanafunzi ni kipaumbele chetu. Tuna zahanati yenye wahudumu wa afya saa 24, mazingira safi na salama, pamoja na huduma ya chakula bora chenye lishe inayozingatia mahitaji ya wanafunzi.

WALIMU, NIDHAMU NA MALEZI

Tuna walimu wenye sifa, weledi na kujitolea katika kufundisha na kulea. Tunasisitiza nidhamu, heshima, uadilifu, uzalendo, kumcha Mungu na kuthamini wengine. Pia tunatoa ushauri na mwongozo ili kuhakikisha kila mwanafunzi anapata msaada wa kitaaluma na kijamii.

USHIRIKIANO NA WAZAZI NA JAMII

Tunaamini kuwa mafanikio ya mwanafunzi yanajengwa kwa ushirikiano kati ya shule, mzazi na jamii. Tunadumisha mawasiliano ya karibu na wazazi, huku tukiwahimiza wanafunzi kujifunza utu, upendo, uwajibikaji na kujitolea kwa jamii.

FALSAFA YETU — UTAVUNA ULICHOPANDA

Tunaamini kuwa elimu bora si ufaulu wa mitihani pekee, bali ni kumjenga mwanafunzi kitaaluma, kimwili, kijamii, kihisia na kiroho. Dhamira yetu ni kulea kizazi chenye maarifa, maadili, kujiamini na uwezo wa kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

DSM GREEN ACRES SCHOOLS

O-Level and A-Level Secondary Schools
Located at Salasala - Mbezi Beach off Bagamoyo Road
Email: info@greenacres.ac.tz | **Website:**www.greenacres.ac.tz
P.O. BOX 105177, DAR ES SALAAM
Phone: +255 754 306 598 | +255 739 999 926 | +255 782 128 633 | +255 765 172 199

MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA BWENI – 2027 [Kidato cha Kwanza hadi cha Nne]

Wazazi/Walezi Wapendwa,

Tunawashukuru kwa kuichagua DSM Green Acres Secondary School kwa ajili ya elimu na malezi ya mtoto wenu. Tafadhali someni maelekezo yafuatayo ili kukamilisha taratibu za kujiunga na kujiandaa kwa mwaka wa masomo 2027.

1. USAJILI NA MASUALA YA TAALUMA

Maelezo	Kiasi (TZS)
Fomu ya maombi na usaili	20,000
Ada ya usajili	30,000
Uchunguzi wa afya	15,000

Muhimu: Wanafunzi wa uhamisho wawasilishe nyaraka husika na taarifa za kitaaluma. Kila mwanafunzi achangie ream moja ya karatasi kwa robo mwaka (ream 4 kwa mwaka).

2. ADA YA SHULE (TZS)

Kidato	Ada ya Robo Mwaka	Ada ya Mwaka
Kidato cha 1	700,000	2,800,000
Kidato cha 2	775,000	3,100,000
Kidato cha 3	875,000	3,500,000
Kidato cha 4	900,000	3,600,000

Utaratibu wa Malipo: Ada inaweza kulipwa kwa mwaka mzima au kwa awamu nne za robo mwaka.

Akaunti ya Ada: NMB Bank. **Jina:** DSM GREEN ACRES SECONDARY SCHOOL. **Namba:** 23110001503

3. MICHANGO MINGINE

Michango ifuatayo hulipwa katika robo ya kwanza ya mwaka wa masomo.

Mchango	Kidato 1	Kidato 2	Kidato 3	Kidato 4
Mitihani	50,000	100,000	100,000	150,000
Programu ya Juni	—	250,000	—	250,000
Mahafali	25,000	25,000	25,000	200,000
Jumla	**75,000**	**375,000**	**125,000**	**600,000**

Bima ya Afya (NHIF): TZS 50,400 kwa mwaka. Ni lazima kila mwanafunzi wa bweni awe na bima ya afya. Malipo ya bima hufanyika shuleni.

4. SARE NA VIFAA VYA SHULE

Sare / Kifaa	Kiasi (TZS)
Sare za shule (jozi 4)	260,000
Fulana (jozi 2)	50,000
Tai (1)	10,000
Mashuka (jozi 2)	40,000
Godoro (1)	70,000
Sweta (1)	25,000
Soksi (jozi 2)	10,000
JUMLA	**465,000**

Sare na vifaa vilivyoorodheshwa vinapatikana katika duka la shule. Malipo yake hufanyika kwa fedha taslimu dukani.

5. MAHITAJI YA DARASANI

Gharama ya kifurushi: TZS 65,000

Kifurushi kinajumuisha madaftari makubwa 13 (Counter Books, Quire 3), madaftari madogo 5 (kurasa 80), mkebe wa hesabu, rula ya sentimita 30, kalamu na penseli za kutosha, faili la kuhifadhia nyaraka (Box File) na daftari la grafu (Graph Pad).

6. VIFAA BINAFSI VYA MWANAFUNZI

Kila mwanafunzi wa bweni anatakiwa kufika shuleni akiwa na mahitaji yafuatayo:

- Traksuti ya rangi ya bluu (Chelsea Blue)
- Viatu vyeusi vya ngozi – jozi 1
- Raba nyeupe za michezo – jozi 1
- Viatu vya wazi vyeusi vya kuvaa bwenini – jozi 1
- Nguo za kulalia – jozi 2
- Nguo za ndani – jozi 6
- Mkanda mweusi (kwa wavulana)
- Ndala za kuogea
- Begi la kubebea madaftari
- Miswaki 6 na dawa ya meno (500 g)
- Mafuta ya kupaka mwilini (500 g)
- Sabuni za kuogea – vipande 6
- Sabuni za kufulia za miche – vipande 3
- Sabuni ya unga ya kufulia kwa mkono – kilo 3
- Karatasi za chooni (Toilet Paper) – roli 3
- Taulo
- Kifaa cha kukatia kucha
- Kiwi na brashi ya kusafishia viatu
- Chandarua cha mviringo – 1
- Sanduku au begi kubwa la kuhifadhia nguo (Suitcase)

7. MAELEKEZO MUHIMU KWA WAZAZI

1. **Utambulisho wa Vifaa:** Nguo na vifaa vyote vya mwanafunzi viandikwe jina lake kwa uwazi ili kuepusha kupotea au kuchanganyika.
2. **Malipo:** Ada na michango yote ilipwe kupitia akaunti rasmi zilizoelekezwa na shule. Malipo ya sare hufanyika katika duka la shule.
3. **Maandalizi:** Mzazi au mlezi ahakikishe mwanafunzi anakamilisha mahitaji yote kabla ya kuripoti shuleni.
4. **Afya:** Wazazi wanapaswa kutoa taarifa kwa uongozi wa shule kuhusu changamoto zozote za kiafya, matumizi ya dawa au mahitaji maalumu ya mtoto.
5. **Ushirikiano:** Tunawahimiza wazazi na walezi kushirikiana na shule katika kuhakikisha nidhamu, usalama, ustawi na maendeleo bora ya mwanafunzi.

8. MAWASILIANO

Kwa ufafanuzi au msaada zaidi, tafadhali wasiliana nasi:
Mkuu wa Shule: +255 739 999 926 **Dawati la Maulizo:** +255 782 128 633

Tunawakaribisha kwa moyo mkunjufu katika familia ya Green Acres. Tunatarajia kushirikiana nanyi katika kumjengea mtoto wetu msingi imara wa elimu, nidhamu, maadili na mafanikio.